

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**  
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI**

MKANGALE SEKONDARI,  
S.L.P 45,  
NKASI-RUKWA.  
11/12/2020

Kumb. Na MKL/SS/NKS/2020/01

Mwanafunzi \_\_\_\_\_

S.L.P \_\_\_\_\_

**NAMANYERE-NKASI.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKANGALE  
ILIOPO WILAYA YA NKASI MWAKA 2021.**

Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.

**1. MAHALI SHULE ILIPO**

- Shule ya sekondari Mkangale ipo mashariki mwa NAMANYERE mji mkuu wilaya ya Nkasi.
- Usafiri wa basi kutoka mjini Namanyere unapatikana katika kituo cha mabasi cha stendi kuu (Mkuyuni) nauli Tsh. \_\_\_\_\_ na usafili wa bodaboda ni Tsh. \_\_\_\_\_
- Muhura wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe \_\_\_\_/\_\_\_\_/20\_\_\_\_ na mwisho wa kuripoti ni tarehe \_\_\_\_/\_\_\_\_/20\_\_\_\_

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

**(a) WAVULANA**

- i) Suruari mbili , moja rangi ya khaki na nyingine rangi ya kijani.
- ii) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.
- iii) Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga kwa kamba.
- iv) Soksi nyeusi jozi mbili.
- v) Sweta la rangi ya zambarau.
- vi) T-shirt zinapatikana shule
- vii) Vifaa vya michezo: Bukta ya bluu,fulana ya bluu, track suit ya blue na raba.

**(b) WASICHANA**

- i) Sketi mbili , moja rangi ya khaki na nyingine rangi ya kijani.
- ii) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.
- iii) Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.
- iv) Soksi nyeupe jozi mbili.
- v) Sweta la rangi ya zambarau.
- vi) T-shirt zinapatikana shule.
- vii) Vifaa vya michezo: Bukta ya bluu,fulana ya bluu, track suit ya blue na raba.
- viii) Hijabu zifanane na sare za shule.

NB: Kuepuka mkanganyiko wa rangi, fuata rangi ya kipande cha kitambaa kilichoambatanishwa kwenye fomu hii.

## 2.2 VIFAA VYA DARASANI

- i) Daftari kubwa tisa (9)-Counter book 2Q
- ii) Daftari ndogo tisa (9)-Msomi page 80
- iii) Mkebe (Mathematical set)
- iv) Kamsi ya Kiswahili na Dictionari ya kiingereza
- v) Begi la kubebea daftari.

## 2.3 CHAKULA

- i) Mahindi debe mbili kwa mwaka
- ii) Maharage sado tatu kwa mwaka
- iii) Mafuta ya kupikia lita moja
- iv) Tsh. 15,000/= kwa mwaka

NB: Fedha za chakula ziwekwe benki katika akaunti namba **6201100044 NMB**, Jina la akaunti ni SHULE YA SEKONDARI MKANGALE.

## 2.4 USAFI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Mwaafunzi anatakiwa aje na vitu vifuatavyo;

- i) Mche mmoja wa mti kwaajili ya kupanda. Mche huo unaweza kuwa wa matunda au mbao
- ii) Ufagio kwaajili ya usafi wa mazingira.

## 3. SHERIA ZA SHULE

3.1: Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978, aidha inazingatia miongozo inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia mabo yamsingi kama ifuatavyo;

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambom la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- c) Kufanya kwa bidii shughuli zote za shule utakazo pewa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule nakuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule.
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- h) Kutunza mali za umma.

3.2: Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule:

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile *bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k*
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau bendera ya Taifa
- h) Kuoja au kuolewa
- i) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, kuongoza na kuchochea mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

4. Mambo mengine ya msingi yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi;
- a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara atakaporipoti shuleni.
  - b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai
  - c) Mkataba wa mzazi wa kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule, pia kumhudumia mwanafunzi na kufuatilia nidhamu na maendeleo yake.
5. Siku ya kuripoti mwanafunzi aletwe/aje na mzazi au mlezi wake.

TAFADHARI SOMA KWA UMAKINI MAELEKEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

